

TAI WANAKUSANYIKA PAMOJA! Tarehe 24/10/2026. Jumamosi.

Wapendwa Waaminifu katika Kristo Yesu,

Tunao wakati mtukufu jinsi gani. Tunayo matarajio makubwa kila wiki tunapoungana pamoja kwenye Sauti Yake. Akili zetu za kiroho hazijachanganyikiwa. TUNAJUA Yeye ni Nani haswa. TUNAJUA kabisa-kabisa Yeye ni nini. TUNAJUA kabisa-kabisa sisi ni nani; familia moja kubwa PAMOJA NAYE!

"Yeye alimjalilia mwanadamu kuwa mungu mdogo." Kwa sababu Yeye ni Mungu Baba, na Yeye alimfanya mwanadamu kuwa mungu mdogo, kwa hiyo Yeye si anayeishi peke yake tena, Yeye anaishi na familia Yake. Elah, Elah, Elohim. Naam, sasa Yeye ni Yehova. Yehova, likimaanisha "Yeye aishiye pamoja na familia Yake."

Familia ya Bibi-arusi Wake inakamilishwa na Sauti ya Yehova Mwenyewe. Yeye ametufundisha jinsi ya kupigana na kila adui anayetushambulia; jinsi tunavyoweza kumshinda na kumweza kwa Neno, kwa sababu Neno Lake linaishi na kukaa ndani yetu. Alituhakikishia, "SISI NI NENO". Kwa hivyo chochote tunachoomba kwa Jina Lake, twaweza kukipokea kama tukiamini....NASI TUNAAMINI!

Yeye amenena na kutufunulia sisi jinsi ya kufikia kimo cha wanaume na wanawake wakamilifu ili tuweze kuwa makao Yeye anayoishi. Yeye ali honk na Aka honk ili kumkusanya Bibi-arusi Wake mpendwa pamoja ili kutujulisha kwamba Yeye ndiye Kiongozi wetu, na Yeye alikuwa akituongoza na kutuelekeza kupitia malaika-kiongozi Wake wa duniani, William Marrion Branham.

Sasa Yeye analo somo lingine maalum analotaka kutufundisha sisi na kutufunulia. Yeye anataka kutangaza kwamba sisi ni watoto Wake wenye mamlaka. Jina letu ni zuri tu kama Jina Lake Yeye. Tumetoka Kanaani, kutoka ulimwenguni, na SASA tumeketi pamoja katika ulimwengu wa roho, tukila ile Mana iliyofichwa, iliyohifadhiwa.

Sasa Yeye atatueleza kile tunachopaswa kufanya ili tuweze kuwa tayari kwa Ujumbe Wake unaofuata, na kile kinachoweza kutukia endapo tukifanya hivyo.

Yatupasa tuwe tumeomba vya kutosha na kuwa tayari kwa Ujumbe; Tukusanyike wenyewe pamoja kama watakatifu ili kuisikia Sauti Yake, Tumebatizwa na Roho Mtakatifu, Tukajazwa baraka za Mungu; Hakuna mawazo mabaya; Hakuna neno dhidi ya kila mmoja wetu; Tukizungumza katika upendo na upatanifu; Tuwe katika nia moja, mahali pamoja katika mahali pa Mbinguni chini ya hali ya Kimbinguni; Dhambi zetu zote zikiwa chini ya Damu, katika ibada kamilifu; Mikono na mioyo yetu imeinuliwa kwa Mungu, tukiabudu pamoja katika ulimwengu wa roho.

Tukiayafanya mambo haya, haya ndiyo yatakayotukia Jumapili hii:

- Uponyaji wa Kiungu
- Kutangulia kujua
- Ufunuo
- Maono
- Nguvu
- Tafsiri
- Hekima
- Maarifa
- Baraka za Kimbinguni
- Furaha isiyoneneka na iliyojawa na Utukufu

Kila moyo utajazwa na Roho. Ndipo kutakuja ghafla toka Mbinguni uvumi kama wa upepo wa nguvu ukienda kasi na Yeye atatubariki kwa baraka zote za rohani.

Hilo ndilo litakalotukia Jumapili hii saa 6:00 MCHANA, masaa ya Jeffersonville, ambapo Mungu amepaandaa mahali maalum ambapo Bibi-arusi anaweza kukusanyika pamoja kuisikia Sauti Yake kwa moyo mmoja, mahali pamoja, huku mikono na mioyo yetu ikiinuliwa kwa Mungu, tukiabudu pamoja katika hali ya Kimbinguni.

Ndugu. Joseph Branham

Ujumbe: ***Kufanywa Wana Wenye Mamlaka #1 60-0515E***

Maandiko:

Yoeli 2:28

Waefeso 1:1-5

1 Wakorintho 12:13

1 Petro 1:20

Ufunuo 17:8

Ufunuo 13